

TAARIFA KWA UMMA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Malawi kwa pamoja, wanaandaa Kongamano kubwa la Biashara na Uwekezaji litakalofanyika tarehe 26 hadi 27 Julai, 2018 Mjini Mbeya. Kama sehemu ya maandalizi ya Kongamano hilo, Mhe. Amos Gabriel Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya jana tarehe 20 Machi, 2018 aliongoza Kikao cha Viongozi cha Maandalizi ya Kongamano hilo ambacho kilihudhuriwa na Mabalazi wa Nchi hizo mbili ambao ni Mhe. Hawa Olga Ndilowe Balozi wa Malawi Nchini Tanzania na Mhe. Benedict Martin Mashiba, Balozi wa Tanzania Nchini Malawi. Kikao hicho kilichohudhuriwa na Bw. Edwin Rutageruka Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ambao ndio Waratibu wa Maandalizi kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali na Sekta Binafsi.

Mhe. Makalla alieleza kuwa Kongamano hilo ni matokeo ya Kikao cha pamoja kilichofanyika Mjini Lilongwe Nchini Malawi Mwaka 2017 ambacho pamoja na masuala mengine kiliazimia kuongeza biashara na kuimarisha uhusiano wa kiuchumi baina ya Tanzania na Malawi. Kadhalika, alieleza kuwa Kongamano linaloandaliwa litawawezesha Wafanyabiashara na Wawekezaji wa Tanzania na Malawi kukutana, kubadilishana uzoefu na kuangalia fursa zilizopo katika nchi zao.

"Tumeanza kufungua milango, ambapo tayari tumetengeneza meli za mizigo ambazo zinafanya safari kutoka Ruvuma hadi Malawi na pia tuna mipango ya kujenga "One Stop Border Post" katika Mpaka wa Kasumulu ili kurahisisha na kuondoa urasimu katika ufanyaji biashara kwenye mipaka na kujenga bandari kavu Mkoani Mbeya itakayowarahisishia Wafanyabiashara wa Malawi kupokea bidhaa moja kwa moja kutoka Bandari ya Dar es Salaam. Hatua hizi zitazinfuisha Tanzania na Malawi kiuchumi." alieleza Mhe. Makalla.

Mhe. Hawa Olga Ndilowe Balozi wa Malawi Nchini Tanzania alieleza kufurahishwa kwake na kupongeza uamuzi wa Tanzania kuwa mwenyeji wa Kongamano hilo. Mhe. Ndilowe alisisitiza kuwa Kongamano litaongeza ukuaji wa biashara na uwekezaji na hivyo kuchangia kuboresha maisha ya Wananchi wa pande zote mbili. Balozi huyo aliahidi kutoa ushirikiano wa hali juu katika kufanikisha maandalizi ya ushiriki wa nchi yake katika Kongamano hilo.

Nae Mhe. Benedict Martin Mashiba, Balozi wa Tanzania Nchini Malawi alisema kuwa nchi za Tanzania na Malawi ni majirani kihistoria na kijiografia hivyo Kongamano hilo litadumisha uhusiano uliopo na kuendelea kukuza uhusiano wa kibiashara kati ya nchi hizi mbili ukizingatia Tanzania ina viwanda vingi hivyo bidhaa nyingi zitaingia nchini Malawi.

Kwa upande wake, Bw Edwin Rutageruka, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ambao ndio waratibu wa Kongamano hilo, amesema kwa muda mrefu sana nchi hizi mbili zimekuwa zikifanya biashara kwa pamoja, ingawa nyingi zimekuwa katika mfumo usio rasmi. Aidha, alieleza kuwa Wafanyabiashara wa nchi hizi mbili wamekuwa wakishiriki kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) na Maonesho ya Kimataifa ya Malawi (MITF). Vile vile alisisitiza kuwa, kwa kuwepo kwa "One Stop Border Post" kwenye mpaka wa Kasumulu kutarahisisha biashara kwa wafanyabiashara waliopo mpakani ambao wengi wao ni Wanawake ili waweze kurasimisha biashara zao na kuongeza mauzo ya bidhaa zao katika Nchi ya Malawi. Hivyo, alitoa wito Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki Kongamano hilo lenye fursa kubwa.

Imetolewa na:



Edwin N. Rutageruka
Mkurugenzi Mkuu

21 Machi, 2018

All official correspondences should be addressed to the Director General

Mwl. J.K Nyerere Trade Fair Ground, Plot No. 436, Block A, Kilwa Road; P.O Box 5402, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 (0) 22 2850238, Fax:+255 (0)22 2858532, +255 (0) 22 2850239, Email: info@tantrade.or.tz, Web: www.tantrade.or.tz